JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO

SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI CHATO

Kumb. Na. CSS/JOIN/2026….

S.L.P 102,

Email: chatosecschool@yahoo.com,

CHATO.

SIMU: 0282228027

MOB: 0754884134 /0777508424 /0768297767

06th DESEMBA, 2025.

---

Mzazi wa……………………………………………………………………….

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA ELIMU YA SEKONDARI UFUNDI KIDATO CHA I -2026**

**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI CHATO, WILAYA YA CHATO MKOA WA GEITA**

**1.0 Utangulizi**

Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari ya Ufundi Chato mwaka 2026. **Hongera sana** na karibu sana. Shule itafunguliwa Januari 13, 2026 mwisho wa kuripoti ni Januari 30, 2026.

**2. MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya sekondari ya Ufundi Chato ipo mkoani Geita katika wilaya ya Chato umbali wa kilometa tano (5) kutoka stendi kuu ya mabasi jirani na hospitali ya wilaya ya Chato na kituo cha polisi Chato.

**NAMNA YA KUSAFIRI KUFIKA CHATO.**

- Kwa wanaotoka mkoa wa Kigoma,wapande magari ya kwenda Mwanza, wateremkie Bwanga au Bihalamulo na hapo wapande magari ya kwenda Chato wateremkie Chato.
- Wanaotoka mkoa wa Kagera wilaya za; Bukoba, Karagwe, Muleba wapande magari ya kwenda Mwanza wateremkie Chato. Wanaotoka wilaya za Ngara na Biharamulo wapande magari ya kuja Chato.
- Kwa wanaotoka mikoa ya Mara, Arusha, Simiyu, Dodoma, Singida, Manyara, Kilimanjaro, Dar es salaam, wapande magari yanayokwenda Mwanza, wakifika Mwanza wapande magari yaendayo Bukoba wateremkie Chato. Vilevile wanaotokea mikoa tajwa hapo juu isipokuwa Mara na Simiyu wanaweza kufika shuleni kupitia njia ya Kahama mabasi yaendayo Bukoba - wateremkie Runzewe wapande magari ya Bwanga kisha magari ya Chato. **KARIBU SANA.**

## 3. SHERIA ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978, pia inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini.

Hivyo kwa kipindi chote utakapokuwa mwanafunzi wa shule hii,utatakiwa kushika na kuheshimu sheria,kanuni na taratibu zote za shule ukiwa ndani na nje ya shule **kwani utakuwa ukiiwakilisha shule popote utakapokuwa. Kutokujuasheria hakutakuwa kinga ya kutokuchukuliwa hatua stahiki**.

## 4. SARE YA SHULE

Wakati wote wa muda wa masomo mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule ambayo ni suruali nyeusi na shati nyeupe (mikono mifupi)- wavulana, sketi nyeusi na shati nyeupe mikono mifupi - wasichana na T-sheti ya shule kwa wote baada ya muda wa masomo, siku za sikukuu pamoja na Jumamosi na Jumapili. Aidha wanafunzi watavaa track suit kipindi cha michezo na dharula mbalimbali.

**Kwa sababu yoyote ile mwanafunzi haruhusiwi kumiliki au kuvaa nguo za kiraia (asije nazo kabisa).**

Pamoja na barua hii naambatisha viambatisho vifuatavyo. (a) Orodha ya mahitaji ya shule, ( b) sheria za shule,

(c) Taratibu na kanuni za shule, (d) Taarifa binafsi ya mwanafunzi, (e) Fomu ya hospitali , (f) Fomu ya mzazi/mlezi

**MATIBABU**

**Gharama zote za matibabu zitagharamiwa na mzazi. Hivyo wanafunzi wote wenye bima za afya za NHIF waje nazo. Kwa wale wasiokuwa nazo wanatakiwa kuja na shilingi 50,400/= na picha moja (1) ya passport size ili mtoto akatiwe bima ya NHIF kupitia ofisi za Bima ya afya mkoa wa Geita. Bima hii itamuwezesha mwanao kutibiwa hospitali ya aina yoyote nchini zikiwemo na hospitali za Rufaa. Ikumbukwe kuwa bima hii hulipiwa kila mwaka kwa wale ambao wana bima ambazo hazipo katika mfumo wa makato kwa watumishi wa umma.**

**CHATO SEKONDARI: ELIMU NA KAZI.**

THE HEAD OF SCHOOL
CHATO TECHNICAL SECONDARY SCHOOL
P.O.Box 102, CHATO.

…………

***SELEMA M. BERNARDO***

***MKUUWASHULE***

## MAHITAJI NA SARE YA SHULE

A: WAVULANA

- ✓ Suruali mbili nyeusi za kushona **zisizobana mwili (modal)** zenye malinda 2 na ‘turn up’
- ✓ Mashati meupe mawili ya mikono mifupi..
- ✓ Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu wala shingo ndefu.
- ✓ Mkanda mweusi wa suruali usio na chuma kikubwa au chenye maandishi.
- ✓ Soksi jozi mbili rangi nyeupe.
- ✓ Sweta rangi ya bluu yenye nembo ya shule ataipata shuleni.
- ✓ T-shirt moja yenye nembo ya shule (inapatikana shuleni)
- ✓ Pensi /bukta za kuvalia ndani 3
- ✓ Chupi au boksa 6
- ✓ Vest /fulana nyeupe 4
- ✓ Godoro imara futi 2 ½ kwa futi 6
- ✓ Shuka 2 rangi ya bluu bahari kwa ajili ya kutandika na kujifunika.
- ✓ Chandarua ya 4/6 rangi nyeupe na foronya/mto rangi ya bluu.
- ✓ Ndoo mbili lita 10 kwa ajili ya kuchotea maji ya kuoga na matumizi mengine.
- ✓ Kidumu cha lita 5 kwa ajili ya maji ya kunywa.
- ✓ Sahani, bakuli, kikombe, na kijiko kwa ajili ya chakula.
- ✓ Kandambili nyeusi kwa ajili ya kuogea **tu**.
- ✓ Taulo kwa ajili ya kuogea
- ✓ Vitambaa vya mkononi 4
- ✓ Mswaki, sabuni ya kufulia na kuogea, dawa ya meno, mafuta ya kujipaka, dawa ya viatu na kitana.
- ✓ Raba nyeupe jozi moja kwa ajili ya michezo.
- ✓ Nguo za michezo **Track suit rangi ya kijani kibichi (**zinapatikana shuleni)
- ✓ Ufagio wa plastiki wa dukani (soft/ hard broom), ufagio wa chelewa, jembe na mpini kwa ajili ya usafi wa nje , ufagio wa raba (mopper) kwa ajili kudekia.
- ✓ Nywele ziwe fupi daima.
- ✓ Tochi yenye betri au taa ya sola.
- ✓ Sanduku la chuma au mbao (tranker) kwa ajili ya kutunzia nguo na vifaa vya mwanafunzi.
- ✓ Boksi moja la vibanio vya nguo
- ✓ Ream mbili za karatasi kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo (michoro) na mitihani ya majaribio

**B: WASICHANA**

- ✓ Shati mbili nyeupe (tetron) za mikono mifupi zisizo na urembo wa aina yoyote ile.
- ✓ Sketi mbili nyeusi zenye marinda ya wastani 12 na yasiyozidi 20 na mkanda wa sketi (Belt) uwe inchi 2 tu. Sketi ziwe ndefu zenye kukaribia kisigino (cm 50 baada ya magoti). Kitambaa kiwe kizito (cha suruali) kisiwe laini cha kutepeta (sukari sukari).
- ✓ Viatu vya **ngozi vyeusi visivyo na visigino virefu wala urembo wowote na viwe vya kufunga na kamba wala visiwe na shingo ndefu.**
- ✓ Soksi ndefu (stocking) za rangi nyeupe bila rangi nyingine yoyote (bila doa).
- ✓ Mswaki, sabuni za kufulia na kuogea, dawa ya meno, mafuta ya kujipaka, dawa ya viatu na kitana.
- ✓ Sweta rangi ya bluu yenye nembo ya shule ataipata shuleni.
- ✓ Rangi ya hijab ifanane na sare ya shule (angalia kiambatisho cha mshono).
- ✓ Gauni rangi ya bluu bahari kwa ajili ya kazi za nje ya darasa na kushindia (itashonewa shuleni).
- ✓ Godoro imara futi 2½ kwa futi 6
- ✓ Shuka 2 rangi ya pink kwa ajili ya kutandika na kujifunika.
- ✓ Tight au underskirtt zisizopungua 6 (mpya)
- ✓ Chupi zisizopungua 8 (mpya)
- ✓ Vest /fulana nyeupe au spice 6 (mpya)
- ✓ Vitambaa vya mkononi 4
- ✓ Doti ya kitenge au khanga na taulo kwa ajili ya kuogea.
- ✓ Chandarua ya duara 4/6 rangi nyeupe na foronya/mto rangi ya bluu.
- ✓ Ndoo mbili lita 10 kwa ajili ya kuchotea maji ya kuoga na matumizi mengine.

- ✓ Kidumu cha lita 5 kwa ajili ya maji ya kunywa.
- ✓ Vifaa vya dharula kwa mtoto wa kike.
- ✓ Sahani,bakuli,kikombe,na kijiko kwa ajili ya chakula.
- ✓ Kandambili nyeusi kwa ajili ya kuogea **tu**.
- ✓ Raba rangi nyeupe jozi moja kwa ajili ya michezo.
- ✓ Nguo za michezo **Track suit rangi ya kijani kibichi (**zinapatikana shuleni)
- ✓ Ufagio wa plastiki wa dukani (soft/ hard broom), ufagio wa chelewa wenye mpini kwa ajili ya usafi wa nje ,ufagio wa raba (mopper) kwa ajili kudekia, jembe na mpini kwa ajili ya usafi wa nje.
- ✓ **Nywele ziwe fupi daima.**
- ✓ Tochi yenye betri au taa ya sola.
- ✓ T-shirt moja yenye nembo ya shule (inapatikana shuleni)
- ✓ Sanduku la chuma au mbao (tranker) kwa ajili ya kutunzia nguo na vifaa vya mwanafunzi.
- ✓ Boksi moja la vibanio vya nguo
- ✓ Ream mbili za karatasi kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo (michoro) na mitihani ya majaribio.

## FANI NA MAHITAJI YA DARASANI

**Shule yetu ina fani Nne (4) za masomo ya ufundi Mkondo wa Amali kama ifuatavyo:**

**i**) Masonry and Bick laying

ii) Motor Vehicle Mechanics

iii) Electrical Installation na

iv) Solar Power Installation.

**MUHIMU : MWANAFUNZI ANAPORIPOTI SHULENI AWE AMECHAGUA FANI MOJA KATI YA NNE HAPO JUU AMBAYO ATASOMA NA KUSAJILIWA.**

### (A) VIFAA VYA FANI NA TAALUMA.

***WANAFUNZI WOTE FANI ZA UFUNDI LAZIMA***: Ovaroli la rangi ya Dark Blue na **Safety Boot** (Zinapatikana Shuleni) ZINGATIA AJE NA **OVAROLI** NA SIO **OVERCOAT.**

(i) Madaftari makubwa kumi na sita (16), counter books quire three.
(ii) Mkebe wa vifaa vya hisabati (Mathematical instrument set).
(iii) Mathematical table (Four figure) -Uandike jina lako katika kitabu hiki.
(iv) Kamusi (English -Swahili Dictionary)-Uandike jina lako katika kitabu hiki.

**NB:** Kwa Wanafunzi watakao chagua fani ya MASONRY & BRICKLAYING pia Waje na Rainy Boot bila kusahau Mahitaji mengine yote tajwa hapo juu.

***Kiambatisho (b)***

## 3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 10 ya mwaka 2002. Aidha shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na mwanafunzi atapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi ,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya darasa kulingana na ratiba ya shule ni lazima;

(c) Kushiriki kwa makini katika kujisomea shuleni na nyumbani (preparation);

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na zingine atakazopewa ;

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo;

(f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule;

(g) Ni lazima utakaporipoti shuleni ushiriki zoezi la kupanda mti mmoja na kuutunza

(h) Kuvaa sale kwa usahihi wakati wote unaotakiwa kwani popote utakapokuwa utakuwa ukiiwakilisha shule; (i)

Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote ;

(j) Kutunza mali ya umma **(uharibifu wowote wa mali ya umma mzazi atawajibika kulipa)**

(k) Kusimama na kusalimia walimu,wageni na watu wote wanaokuzidi umri.

(l) Kuzingatia usalama kwanza uwapo katika maeneo ya karakana.

(m) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na vifaa vya aina yoyote vya ufundi hapa shuleni, vikikamatwa vifaa hivyo vitachukuliwa kama mali ya shule.

**3.1 UHAMISHO**

Uhamisho usio wa lazima au wa holela kwa wanafunzi katika shule hii hautakubaliwa. Uhamisho utakaotolewa ni ule wa lazima na halali wenye viambatanisho vya sababu za kuomba uhamisho huo. Na uhamisho huo utatolewa mara mbili kwa mwaka yaani mwezi Juni na mwezi Disemba. Hivyo utaijulisha shule mapema ili taratibu za uhamisho zifanyike kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**KARIBUNI SANA**

**CHATO SEKONDARI :ELIMU NA KAZI**

THE HEAD OF SCHOOL
CHATO TECHNICAL SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 102, CHATO.

***SELEMA M.BERNARDO***

***MKUU WA SHULE***

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO**

**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI CHATO**

**SHERIA ZA SHULE**

**(a) TARATIBU NA KANUNI ZA SHULE**

1.**HESHIMA**: Kila mwanafunzi anatakiwa kwanza kujiheshimu mwenyewe, kuwaheshimu walimu,wazazi/walezi,wageni na viongozi kwa ujumla.

2**. MAWASILIANO**:Kingereza ndiyo lugha pekee ya mawasiliano hapa shuleni, hivyo mwanafunzi haruhusuwi kuwasiliana kwa lugha nyingine yoyote isipokuwa tu wakati wa midaharo ya Kiswahili.

3.**USAFI**: Kila mwanafunzi anatakiwa kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule kwa ujumla.

4.**RATIBA YA SHULE**:

Kila mwanafunzi anapaswa kuheshimu ratiba ya shule.Mwanafunzi haruhusiwi kuwa nje ya mazingira ya shule bila ruhusa ya **maandishi** kutoka kwa uongozi wa shule. Aidha mwanafunzi anatakiwa kuwahi darasani na katika shughuli mbalimbali za shule ikiwa ni pamoja na kutii **kengere.**

**(b) MAKOSA YA KUFUKUZWA SHULE MWANAFUNZI**.

1. Wizi wa aina yoyote.

2.Uasherati, ushoga na ubakaji.

3. Ulevi wa pombe/madawa ya kulevya kama vile mirungi,kuber,bangi n.k

4. Kupiga/kupigana/kutoa lugha chafu kwa wanafunzi/walimu/jamii.

5.Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

6.Kudharau bendera ya Taifa.

7. Kuoa/ kuolewa, kubeba mimba/kumpa mimba msichana.

8.Kugoma, kuchochea/kuongoza mgomo na kuvuruga amani na usalama shuleni/jamii.

9.**Mwanafunzi kumiliki line/simu ya mkononi.**

10.Udanganyifu wa aina yoyote katika mitihani.

11.Kugomea adhabu yoyote halali.

12.Utoro/kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa.

**(c) MAKOSA YAFUATAYO YAKIJIRUDIA YATASABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1.Utoro wa aina yoyote ile

2.Kuchelewa kufika shuleni na katika shughuli mbalimbali za shule.

3. Kutokuvaa sale rasmi ya shule kulingana na ratiba ya shule

4. Uchafu wa mwili (kutokunyoa ndevu/nywele,kutokuoga /kutokufua n.k )

## ANGALIZO :

***Mwanafunzi atakayebainika/ kukamatwa na simu au line ya simu atatozwa faini ya shilingi laki mbili tu (TSH. 200,000/=) Hivyo mzazi hakikisha mwanao hamiliki simu kwa namna yoyote ile ili kuepuka kuisababishia familia hasara isiyo ya lazima.***

# HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO

# SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI CHATO

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

***FOMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI (kwa uangalizi wa mzazi)***

1. Jina kamili ……………………………………………………………………………………………… 2

(a)Tarehe ya kuzaliwa……..…………………………………………………………………………

(b)Mahali alipozaliwa ………………………………………………………………………………

3. (a) Dini ………………………………………………………………………………………………

(b) Dhehebu ………………………………………………………………………………………

4. (a) Uraia …………………………………………………………………………………………......

(b) Kama siyo raia wa Tanzania taja uraia wako ………………………………………………………

5. Shule ya msingi uliyotoka ……………………………………………………………………………… 6. (a) Jina kamili la mzazi /mlezi ……………………………………………………………………… (b) Anwani ya mzazi/mlezi …………………………………………………………………………

(c) Kazi ya mzazi/mlezi ……………………………………………………………………………

(d) Kituo chake cha kazi ……………………………………………………………………………

(e) Namba ya simu ya mzazi /mlezi………………………………………………………………………

7. (a) Mahalia anapoishi ………………………………………………………………………………

(b) Jina la mwenyekiti wa kitongoji/mtaa ……………………………………………………………

8. (a) Je, unaishi na nani? Taja jina kamili ………………………………………………………………

(b) Je,una uhusihano gani na huyu uliyemtaja?...............................................................................................

9. Ni yatima/si yatima ……………………………………………………………………......................

10. Kama ni yatima mzazi yupi aliyefariki:mama/baba/wote …………………………………………

……………… ………………

Saini Tarehe

***Kiambatisho (e)***

CHATO DISTRICT COUNCIL

CHATO TECHNICAL SECONDARY SCHOOL,

P.O.BOX 102,

**CHATO.**

06/12/2025

MEDICAL OFFICER IN CHARGE

………………………………………,

……………………………………….,

**RE: MEDICAL EXAMINATION OF________________________________**

Please examine the above named student as to his physical/mental fitness/unfitness for admission as full time student of Chato Technical Secondary School for academic year 2025.

The examination should include the following categories: Eye sight, Hearing, Epilepsy, Urine, UPT(Girls),Venereal disease, Stool and any other body deformations.

…………………

THE HEAD OF SCHOOL
CHATO TECHNICAL SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 102, CHATO.

THE HEADMASTER

THE HEADMASTER, MEDICAL INCHARGE ,

CHATO SECONDARY SCHOOL, …………………………..,

P.O.BOX 102, …………………………….

**CHATO.** **Date……………………**

**RE: MEDICAL EXAMINATION RESULTS**

I have examined the above named student and found him with the following disease/ impairment/disabilities:
Eye sight………………………………………………………………………………………………

Urine examination………………………………………………………………………………

Pregnancy (UPT)…………………………………………………………………………………

Hearing…………………………………………………………………………………………………

Stool examination………………………………………………………………………………

Speech ……………………………………………………………………………………………..

Venereal diseases…………………………………………………………………………………

Limbs……………………………………………………………………………………………………

Epilepsy…………………………………………………………………………………………………

Additional information/other serious diseases……………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………………...

Name and signature of attending officer…………..…………………Date…………………………….

Designation……………………………… Official stamp………………………………………..

*Kiambatisho (f)*

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO

**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI CHATO**

**FOMU YA KUKUBALI**

Mzazi/Mlezi wa (Jina la mwanafunzi)

_______________________________

Mimi……………………………………(mwanafunzi) bila shuruti nakubali kutumia nafasi niliyopewa ya kidato cha kwanza **(I-2026)** katika shule ya sekondari Chato. Pia naahidi kutii sheria za shule ikiwa ni pamoja na kuhudhuria shuleni inavyotakiwa,

……………………… …………….

Saini ya mwanafunzi tarehe

Mimi…………………………………………………………………. mzazi /milezi wa……………………………. (jina la mwanafunzi) nimeyasoma masharti yote ya mwanangu kujiunga na shule ya sekondari Chato na ninakubali na kuahidi kwamba mtoto wangu atafuata masharti yote yaliyotajwa katika fomu hii. Pia nitahakikisha kuwa mwanangu anahudhuria masomo inavyotakiwa na anamaliza elimu ya kidato cha nne kwa kuwajibika kumpatia mahitaji ya shule pamoja na kushirikiana na uongozi wa shule katika kumlea kitaaluma na kinidhamu.

…………………….. ………………….

Saini ya mzazi/Mlezi Tarehe






**SARE YA SHULE – WAVULANA** **OVERALL KWA WASICHANA NA WAVULANA**






MBELE
BARAZA KUU LA WAISLAMU WA TANZANIA
(THE NATIONAL MUSLIM COUNCIL OF TANZANIA)
KITAMBAA CHEUPE
(JALABIB)
SHATI PANA JEUPE
MIKONO MIREFU
SKETI NDEFU
RANGI YA SHULE
SOKSI NYEUPE
VIATU VYEUSI
NYUMA




**SAFETY BOOT KWA WAVULANA NA WASICHANA**